**VVU/UKIMWI katika Jamhuri ya Dominika**

**Imeandikwa na Yaceibol Ballast**

Jamhuri ya Dominika ni nchi iko katika Caribbean ambayo ina idadi ya wakazi zaidi ya milioni 9. Mji mkuu wake na makao makuu ya serikali yanapatikana katika Santo Domingo de Guzmán. Jamhuri ya Dominika ni nchi inayoendelea ya mapato ya kati, ikitegemea zaidi sekta za kilimo, biashara, huduma, hasaa utalii. Ingawa sekta ya huduma imeimarika kupita sekta ya kilimo kwa kutoa ajira, kilimo bado ni muhimu katika suala la matumizi ya nchi.

Tangu miaka ya 1960, matatizo ya kiuchumi yamesababisha uhamiaji wa watu wengi Marekani, hasa kwa miji mikuu ya pwani ya mashariki. Raia wa Dominican ni moja ya makundi kubwa zaidi miongoni mwa Waamerika Kusini katika Marekani.

**VVU/UKIMWI**

Jamhuri ya Dominika ina watu 120,000 walioathirika na VVU, mara tisa ya jumla ya idadi ya kesi zilizoripotiwa, na katika miaka kumi iliyopita karibu watu 20,000 wamekufa kutokana na ugonjwa wa ukimwi. VVU/UKIMWI ni sababu kuu ya kifo kati ya wanawake waliotimia umri wa kuzaa. Vikundi vya kipato cha chini vina tukio kuu ya ugonjwa huu (asilimia 5 ya watu wazima), miongoni mwa vikundi hivi ni wahamiaji wa Haiti wanaoishi katikavijijini na kufanya kazi katika mashamba makubwa ya miwa. Idadi ya ugonjwa huu miongoni mwa wanawake ambao hushiriki katika biashara ya ngono ni karibu asilimia 8, ingawa katika baadhi ya miji inaweza kufikia kama asilimia 12. Kifua kikuu (TB) ni maambukizi nyemelezi yanayoathiri watu wenye UKIMWI kwa wingi.

Katika asilimia 81 ya kesi za VVU, virusi huenezwa kwa mahusiano ya wapenzi wa jinsia tofauti miongoni mwa watu wenye umri kati ya miaka 15 na 44, kati ya wanawake 4000 waliopatikana na VVU/UKIMWI katika vipimo kabla ya kujifungua, inawezekana kuzaliwa kwa watoto 1300 walioambukizwa. Sababu ya hali hii ni: viwango vya juu vya magonjwa ya zinaa (STIs), viwango vya juu vya kuzaa miongoni mwa vijana na wanawake vijana, na uhamiaji.

**Hatua za Serikali dhidi ya VVU/UKIMWI**

kati ya juhudi za serikali dhidi ya ugonjwa wa VVU/UKIMWI ni:

• Kuzindua amri ya rais ya kiwango cha juu cha taasisi (Tume ya Rais ya UKIMWI, COPRESIDA), ambayo inategemea moja kwa moja Rais na ni jukumu lake ni kuratibu mapambano dhidi ya UKIMWI. COPRESIDA inashughulikia mashirika ya kawaida, ya kibinafsi na ya umma.
• Kudhibiti mada ya VVU/UKIMWI kutokana msimamo wa kitamaduni, kijamii, na mtazamo wa kiuchumi, na kushirikisha sekta mbalimbali na wahusika kwa njia ya kushirikiana na serikali, sekta za kibinafsi na mashirika ya umma, ikiwa ni pamoja na watu walioathirika na virusi vya ukimwi.
• Kuzindua hatua za kudhibit kuenea kwa, kukita ngome na kupanua mikakati yenye mafanikio makubwa, ikiwa ni pamoja na ushauri na upimaji wa hiari, udhibiti wa STIs, kuzuia VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, na utoaji wa tahadhari na usindikaji wa watu walioathirika na VVU ambao wanahitaji tiba kulingana na miongozo.
• Kutilia makini hatua fanisi zaidi katika gharama, na kuongoza mikakati kwaa wakazi wa mazingira magumu zaidi.
• Sheria ya 5593 (1995) hushugulika na mandhari ya VVU / UKIMWI, na ilizinduliwa kuanzisha makala yasiyo na ubaguzi dhidi ya wale ambao wanaishi na virusi.

**Wanawake**

*Wanawake nchini humu huwajibika kupimwa wakati wanapojifungua.*

Wanawake wa Jamhuri ya Dominika hukabiliwa na aina mbalimbali ya kukosekana kwa usawa, ubaguzi na kutengwa kijamii. Licha ya kiwango cha kusoma na ngazi ya elimu ya msingi ya wanaume na wanawake katika Jamhuri ya Dominika kuwa ya juu, wanawake wamewakilishwa kwa sehemu ndogo katika soko la ajira. Wanawake wengi ni waathirika wa unyanyasaji wa nyumbani, huku wakikabiliwa na upungufu mkubwa katika uwezekano wa kushiriki kwa kijamii na harakati zake kwa mujibu wa waume zao, au washirika katika mahusiano ya muda mrefu.

Katika utafiti uliyofanywa mwaka 2002 na Measure DHS + (Survey ENDESA), zaidi ya nusu ya

wanawake waliohojiwa ambao walikuwa na washirika wa kimapenzi wa muda mrefu, walisema kwamba waume zao, au washirika wa kiume, walitaka kuelezwa habari ya shughuli zao kila wakati. Asilimia kumi ya wanawake hawa walisema kwamba waume zao, au washirika wa kiume, walipunguza uwezo wao wa kupata marafiki, na asilimia 11 walisema kuwa walipunguziwa uwezo wa kushirikiana na familia zao.

Upungufu wa mahusiano ya kijamii na katika mahusiano ya muda mrefu unaweza kuwa mwanzo wa ugomvi wa nyumbani, kwa hivyo kusababisha mazingira yanayokubali kwamba wanawake wanapaswa kuwasilisha mamlaka ya wanaume. Utafiti wa ENDESA wa 2002 uligundua kuwa asilimia 24 ya wanawake katika Jamhuri ya Dominica walinyanyaswa kimwili. Utafiti huo umeonyesha kuwa asilimia 27 ya wanawake waliohojiwa walinyanyaswa kimwili, kingono au kihisia kwa mikono ya waume wao au washirika wao, na kwamba asilimia 5 walinyanyaswa kupitia aina zote tatu za unyanyasaji. Kulingana na takwimu za serikali, unyanyasaji ulikuwa sababu kuu ya vifo vya wanawake katika mwaka 2000. Katika mwaka 2003, asilimia 83 ya waathirika wa kike wa mauaji waliuawa na waume zao wa sasa au wa zamani au washirika wa kawaida. Vyama maalumu vya polisi tano tu ndio hupokea malalamiko ya ghasia za ndoa nchini kote (vyama hizi vinaitwa "Friends of the Woman ") na hutumika kama kimbilio pekee la waathirika wa unyanyasaji. Vimya hivi husimamiwa kama NGO.

Wanawake hawapati malipo sawa kwa ajira na pia hawaoati mpango sawa katika sehemu za kazi. Utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia umeonyesha kuwa wanawake asilimia 76 tu ya malipo yaliopatikana kwa wanaume katika ajira (asilimia 63 katika maeneo ya vijijini), na kwamba ajira miongoni mwa wanawake imepunguka mara dufu.

Jamii hulaumu mwanamke wakati mumewe au mpenzi asipokuwa mwaminifu, na kuongeza hofu ya wanawake wengi ya kujulikana wazi kuwa wanaauguza VVU. Hofu hii iko na msingi: sheria juu ya UKIMWI inahitaji kuwa wapenzi ambao umeshapata mahusiano ya ngono wafahamishwe unapopatikana na VVU. Kuna uwezekano mkubwa wa anawake kupimwa VVU, na hivyo basi kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na ufahamu wa hali yao. Kwa hivyo, inawezekana pia wanaohusiana nao wasijue juu ya hali yao. Hii inaimarisha mtazamo kwamba wanawake ndio huleta VVU kwa ndoa au mahusiano mengine.

Katika sekta ya afya, idara ya kupima kabla na baada ya kuambukizwa haina uwezo wa kutosha. Wataalamu wa afya hueneza matokeo ya upimaji wa VVU bila mamlaka, na kukataa au kuchelewa katika huduma za matibabu kwa wanawake wanaoishi na VVU. Watu wengi wanaoishi na VVU katika Jamhuri ya Dominika hukutengwa katika ajira au wanazuiliwa kupata huduma ya afya kutokana na hofu ya unyanyapaa na unyanyasaji.

**Unyanyapaa na Ubaguzi katika Sekta ya Afya**

- Kukataa kuwahudumia wagonjwa wanaoishi na VVU
- Kuchelewa kwa aina nyingine za huduma (chakula, usafi)
- Ukosefu wa huduma kwa wagonjwa katika vitanda
- Uchunguzi uliofanywa bila ridhaa ya mgonjwa
- Ukiukaji wa haki za mgonjwa.
- Uchunguzi au tabia zisizofaa
- Matumizi ya uamuzi wa tahadhari
- Matumizi ya tahadhari nyingi

**Hitimisho**

Serikali hivi karibuni ilitekeleza mfululizo wa hatua ambazo huchangia katika kuzuia VVU/UKIMWI na inastahili kupongezwa. Hata hivyo, haijachukulia kwa umakini kukosekana kwa usawa na ubaguzi wa wanawake, wala kushughulikiwa jambo hili kama sababu ya kuchangia uenezi wa ugonjwa huu. Serikali pia imeshindwa kuonyesha dhamira ya kisiasa kutoa ufumbuzi wa ubaguzi na mateso ya jumla kwa wafanyakazi wanaoishi na VVU/UKIMWI. Sheria juu ya UKIMWI inatafakari adhabu kwa wanaotoa taarifa matokeo ya vipimo bila ruhusa , lakini hizi vikwazo havijatekelezwa.

Mageuzi yanahitajika kwa haraka kuhakikisha kuenea kwa vipimo kabla na baada ya VVU kwa wanaohitaji, na kubuni hatua za kuhakikisha siri ya matokeo na kutovumilia wanao kiuka sheria hii.